Barua ya Shahidi wa Uislamu na Iran; Shahidi Haj Ghasem Soleimani, Kamanda wa Kikosi cha Quds cha Kikosi cha Walinzi wa Mapinduzi ya Kiislamu, kwa binti yake Fatemeh juu ya falsafa ya maisha, jihadi, na hamu ya kuuawa akiwa katika vita vya kuwatete wanyonge na watoto wa waliojaa khofu ulimwengu mzima.

Kwa jina la Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu

Je! Hii ni safari yangu ya mwisho! Au hatima yangu ni kitu kingine? Ila mimi nimeridhika na chochote kile kitakachonikuta katika njia hii. Ninakuandikia barua hii nikiwemo safarini humu, barua ambayo itakuwa ni kumbukumbu kwako pale utakapokuwa mpweke. Au labda pia utapata kitu muhimu ndani yake ambacho utanufaika nacho.

Kila wakati ninapoanza safari huhisi kama vile sitakuona tena.

Mara nyingi njiani, huziwaza nyuso zanu zenye upendo na kuziona mbele ya macho yangu moja baada ya nyengine huku macho yangu yakibubujika machozi. Ninakutamanini mno, Mungu akulindeni.

Ingawa nilikuwa na nafasi ndogo ya kuonyesheni upendo wangu kwenu, na sikuweza kukuonyesheni kina cha upendo wangu nilionao juu yenu. Jee uliwahi kumuona mtu kusimama mbele ya kioo na kuyakabili macho yake kwa kuyahakikishia upendo wake juu ya macho yake! Ni mara chache jambo kama hilo kutokea, ila macho yake ni muhimu mno kwake. Hivyo nyinyi ni macho yangu, ninakupendeni kama ninavyoyapenda macho yangu. Hivyo nitamke au nisitamke, ila nyinyi ni vipenzi vyangu. Zaidi ya miaka ishirini sasa niko katika hali ya wasiwasi juu yenu, huku nanyi mkilala na ndoto za khofu. Kila nilipofikiri kufanya kazi nyengine kuliko hii ili kukutoeni katika hali hii sikuweza. Si kwa sababu labda mimi napenda sana kazi za mfumo wa kiserikali, au labda kwa kupenda ajira, na pia si kwa sababu ya kulazimishwa. Ewe binti yangu katu jambo hilo halipo, mimi sipo tayari kwa ajili ya ajira au kwa kulazimishwa na mtu fulani kukuwekeni katika hali ya khofu, seuze kukulizeni na kukutoweni machozi.

Niliona kila mtu katika ulimwengu huu amechagua njia yake mwenyewe, mmoja ni mwanafunzi na mwingine ni mwalimu, mmoja ni mfanya biashara, na wengine mkulima. Na kuna mamilioni ya njia, au tuseme, kuna njia kwa idadi ya mwanadamu walivyo, na kila mtu amechagua njia yake mwenyewe.

Hapo nilijiuliza; Ni njia gani nilipaswa kuchagua. Nilijifikiria na kukagua maswala kadhaa na kujiuliza, kwanza, njia hii ni ya muda gani na inaishia wapi? Pia ni kiwango gani cha fursa nilichonacho? Na kimsingi malengo hasa ni nini? Ndipo nilipogundua ya kuwa mimi ni wa muda mfupi na kila mtu ni wa muda mfupi. Kila mtu hukaa na kuondoka kwa muda wa siku kadhaa tu. Wengine huishi miaka michache tu, wengine ni miaka kumi, pia wapo wachache wanaofikia miaka mia moja. Lakini kila mtu anaondoka na kila mtu ni wa kupita njia.

Niliona kwamba ningelikuwa nafanya biashara. Basi wisho wake ni kumiliki sarafu zenye kung'ara, nyumba chache na magari machache. Lakini hazina athari wala tija katika hatima yangu na katika mwelekeo wangu huu. Nilidhani nitaishi kwa ajili yako. Niliona kuwa nyinyi ni muhimu na wa thamani sana kwangu, kiasi cha kwamba; ikiwa mna maumivu, maumivu yenu yatafunika mwili mzima.

Mkikutwa na shida, hujikuta nipo katika moto. Mkiniacha siku moja tu, dhamana ya kuishi kwangu itaporomoka. Nilijiuliza vipi ninavyoweza kutatua hofu na wasiwasi huu. Hpo Niliona ya kwamba; ni lazima niungane na yule ambaye ataniponya na kulitatua jambo hili muhimu, na yeye si mwingine ni isipokuwa

Mwenye Ezi Mungu. Thamani na hazina yenu enyi maua ya uhai wangu haiwezi kuhifadhiwa kupitia utajiri na nguvu za kibinadamu. Vinginevyo, basi matajiri na wenye nguvu wangeliweza kujiepushe na kifo, au utajiri wao na nguvu zingelizuia magonjwa au kuyaponya magonjwa yao yasiyotibika na kuwaepusha kuanguka kitandani.

Nimemchagua Mungu na njia yake. Hii ni mara ya kwanza kukiri hukumu hii; Sikutaka kamwe kuwa katika jeshi, sijawahi kupenda kutukuzwa. Katu sifadhilishi kuitwa jina lolote lile zuri kuliku la Qasim, ambalo hulisikia kutwamkwa na kinywa safi cha Basiji Pasdaran (valantia au mfuasi wa kikosi cha jeshi la kujitolea) ambao baadhi yao wameshakufa mashahidi na wengine wapo njiani.

Nilitaka tu kuwa kuitwa jina la Qasim bila kiambishi cha aina yeyote ile. Kwa hivyo, nikatoa wasia wa kuandikwa juu ya kaburi langu; Askari Qasim peke yake bila ya nyongeza yoyote, Wala sio Qasim Soleimani, anayetukuzwa. jambo ambalo litaniengezea mzigo. Ewe kipenzi changu, mimi nilimwomba Mwenye Ezi Mungu aijaze upendo kwake mishipa ya yangu na kapilari zangu zote zinazohimili uhai wangu. Ewe Mola; jaza pendo wako ndani ya uhai wangu. Sikuchagua njia hii kwa ajili ya kuua, wewe unajua ya kuwa, siwezi kustahamili kuona kuku anavyo katwa kichwa. Ikiwa nimeshika silaha, ni kwa ajili ya kusimama dhidi ya muuaji, na sio kuua. Ninajiona kama mwanajeshi katika nyumba ya kila Mwislamu aliye katika hatari, na ningependa Mungu anipe nguvu ya kuweza kutetea wanyonge wote duniani.

Sitatoa maisha yangu kwa ajili ya Uislam wangu mpendwa ambao maisha yangu si chochote si lolote, wala si kwa Mshia aliyeonewa ambaye hana uwezo kuliko mimi, hapana .. lakini ni kwa mtoto aliyejaa khofu na fazaa, asiye na msaada ambaye hana pa kukombilia. Nitampigania mtoto aliyeogopa na kuking'ang'ania kifua cha mama yake na kwa yule anayekimbia na kufukuza huku akikukosa makazi, ambaye ameacha mstari wa damu nyuma yake.

Ewe kipenzi changu, mimi ni mmoja wa askari jeshi ambalo wafuasi wake hawalali na wala halipaswi kulala, ili wengine waweze kulala kwa amani. Wacha amani yangu itolewe muhanga kwa ajili ya amani yao, ili walale kwa amani. Binti yangu mpendwa, unaishi nyumbani kwangu kwa salama na heshima kamili. Nifanye nini kwa ajili ya yule msichana mnyonge ambaye hana sauti ya kilio, na yule mtoto anayelia ambaye hana chochote ... ambaye hana kitu na amepoteza kila kitu. Kwa hivyo nifanye mimi kuwa nadhiri yako na umwachie yeye Allah. Acha niende, nienda tena na tena. Nitawezaje kukaa na kustahamili, hali ya kwamba msafara wangu wote umekwenda na mimi nimebaki nyuma.

Binti yangu we! kwa kweli nimechoka mno. Sijalala kwa kipindi cha miaka thelathini, lakini sitaki kulala tena. Ninaweka chumvi machoni mwangu ili kope langu lisithubutu kuungana ili nisije ghafilika na kusababisha yule mtoto asiye na makimbilio kukatwa kichwa kwa uzembe wangu. Unatarajia nini kutoka kwangu hali ya kwamba; kila nikifikiria huhisi yule msichana mwenye woga na khofu sawa na wewe Narjis na Zainab. Na yule mvulana na kijana mdogo aliyelazwa machinjioni akiwa katika hali ya kukatwa kichwa, ni wewe ni Hussein wangu mimi na ni Ridha wangu mimi. Wataraji nini kutoka kwangu? Je niwe ni mtazamaji, nibaki bila kujali, na niwe ni mfanya biashara asiyejali? Hapana, siwezi kuishi hivi.

Amani na rehema za Allha ziwe juu yenu.